



UJUMBE WA MLEZI WA TDC GLOBAL KWA DIASPORA WATANZANIA

Salaam wana Diaspora wote popote mlipo.

Mlezi wa TDC Global Mhe Dkt. Willibrod P. Slaa anachukua fursa hii kuwakaribisha kwenye fursa nyingi za uwekezaji na biashara nchini Tanzania, wakati tunasubiri sera na sheria za Diaspora zikiandaliwa na serikali. Aidha serikali ya awamu ya sita ipo kwenye hatua nzuri ya kuboresha mazingira ya biashara kwa kufanyia marekebisho hata kabla ya sera rasmi ya Diaspora (ndani ya sera ya Mambo ya Nje) kukamilika. Marekebisho hayo ya sheria mbalimbali yanategemewa kuingia bungeni wakati wowote ikiwa ni pamoja na bunge la Septemba 2021.

Ni imani yangu wana Diaspora tutachukua fursa hiyo. Hata hivyo wako wana Diaspora, ambao tayari hata kwa sheria zilizopo tayari wameanza na wanawekeza Tanzania. Mfano wa hivi karibuni ni Sight Plus Company Limited ambao Tarehe 30 July 2021 wanazindua kliniki ya kisasa ya macho na meno, jijini Dar Es Salaam, na kliniki zingine 2 mikoani, Tanzania. Tukiwa na nia moja inawezekana. Hiyo ni fursa kwa wana Diaspora wenyewe kuwekeza.

Lakini pia Mhe. Dkt Willibrod Slaa anapenda kutukumbusha kuwa, wana Diaspora tunaalikwa kutumia uzoefu wao kushawishi wenye mitaji mikubwa, kwenye nchi zetu za makazi wetu kuwekeza Tanzania. Vilevile hasa katika maeneo ya "Value Chain Addition" katika mazao ya kilimo. Hii itatusaidia Tanzania kupata faida kamili kutokana na rasilimali zetu, mathalani badala ya kuuza nje korosho ghafi tunaweza kupata faida ya mafuta na bidhaa nyingine iwapo korosho zetu karanga zetu, mawese yetu yatachakatwa na viwanda vyetu wenyewe.

Maeneo mengine ya uwekezaji ni katika viwanda vya madawa ya binadamu (Pharmaceuticals) viwanda vya bidhaa za ngozi, mathalani viwanda vya viatu, na kadhalika kwa rasilimali zilizoko nchini.

Tunaweza kuwekeza kwenye kila aina ya viwanda na hivyo kuunga mkono sera ya serikali ya Tanzania ya viwanda. Fursa za uwekezaji Tanzania ni nyingi (Unlimited) na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan yuko katika kutengeneza mazingira bora kwa uwekezaji na biashara.

Karibuni sana wana Diaspora, wenzetu wameonyesha njia. Kumbe hata katika mazingira ya sasa inawezekana kuwekeza Tanzania. Baada ya “Blue Print” kuwa “Translated into Enabling legislation” (yenye kuzingatia mahitaji ya Diaspora), nini kitashindikana wakati taratibu za sera na sheria zinaendelea kwa mchakato “Legislative Ieter”, ambayo kwa kawaida ni mchakato mrefu na wa pole pole. Uwekezaji na biashara ni swala la “Timing”.

Kuanzia tarehe 1 January 2021 mkataba wa “Africa Free Continental Trade Area” uliingia kwenye utekelezaji, na Tanzania ambayo ni “Signatory” ipo kwenye hatua ya kukamilisha taratibu za “Ratification” bungeni. Hii tafsiri yake ni kuwa Afrika punde litakuwa soko moja huru, ni kwa msingi huo wenzetu kutoka nchi nyingine wanawahi kuwekeza kwenye “Location” nzuri. kwa rasilimali za bandari, SGR inayoenda kukamilika kwa kasi kubwa, Mradi wa umeme wa JKN, Airport kubwa ya Msalato Dodoma na mengineyo. Je ni mfanyabiashara yupi atapuuza “Strategic Location “ ya Tanzania kama “Ideal Investment Destination!” Ukiisha kuchelewa utakuwa umechelewa. Ndio msingi wa “Scramble “ tunayoiona sasa. Tukichelewa tusilalamike.

Shime wana Diaspora, iwapo mtahitaji maelezo ya kina mnaweza pia kuwasiliana na Ubalizi wa Tanzania kwenye maeneo yenu ya makazi, au TDC Global ambacho ni kiunganishi cha wana diaspora duniani, au Ubalizi wa Sweden ambao ni Mlezi wa TDC Global. Wakati ni huu! Karibuni sana.

Diaspora na Nyumbani

Mahusiano ya Umma
TDC Global
2021-07-25

2/2

